Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini! Tubuni kwa Allah toba iliyotakasika; huenda Mola wenu Akawafutieni maovu yenu na kuwaingizeni katika Pepo zipitazo mito chini yao, siku ambayo Allah Hatamfedhehesha Mtume na wale walioamini pamoja naye;... Surah 66:9

JUZU 80 No. 215 | JUM.II-RAJ.1440 AH | MEI 2020 | AMMAN 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Utoto na Masomo ya Seyidna Ahmad as

Na **Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani Rabwah, Pakistan**



Kuna methali maarufu ya Kiurdu inayomaanisha kwamba mtu mkubwa anatambulika tangu utotoni. Sawa na methali hii, utoto pia wa Seyyidna Ahmad as. ulikuwa mtakatifu na wenye mng'ao sana. Hakuwa na mazoea ya kushughulikia michezo na mzaha usio na maana pamoja na watoto wengine, wala hakuungana na watoto wengine katika utundu na utukutu. Katika utoto wake safari moja alichunga mbuzi pia kwa muda fulani sawa na suna ya mitume. Ilitokea hivi kwamba safari moja yeye alikaa kwenye kisima nje ya kijiji na akahitaji kuagiza kitu fulani kutoka nyumbani. Akamwambia yule aliyekuwa anachunga mbuzi huko karibu kuwa amletee kitu hicho toka nyumbani. Yeye akasema, Bwana, nani atalinda mbuzi zangu? Akasema, wewe nenda, mimi nitawalinda. Hivyo, akachunga mbuzi zake, na hivyo Mwenyezi Mungu Alimjalia kutimiza suna ya mitume kwa njia hii. (Siratul Mahdi, sehemu ya kwanza, uk. 250, chapa ya pili)

Mwandishi wa maisha yake na mwanahistoria wa Jumuiya, Hadhrat Sheikh Yakub Ali Irfani ra., ameeleza tukio moja la ajabu la utoto wake kwamba katika umri wake mdogo alikuwa anamwambia mwenzake (ambaye baadaye aliolewa naye) kwamba niombee kwamba Mungu Anijalie sala. (Hayatun Nabii, Jl. 1, Na. 2, uk. 158)

Haya yalikuwa matokeo ya tabia yake safi na mazoea yake mazuri na mienendo mizuri kwamba mtu yeyote aliyemwangalia kwa jicho la busara akawa anampenda.

Mwalimu mmoja wa Kiahmadiya, Mian Muhammad Husain wa Balochistan, anasimulia: "Maulawii Burhanud Din ra. aliniambia kwamba safari moja Hadhrat Masihi Mau'udi as. katika utoto wake alimwendea Maulawii Ghulam Rasul wa Qila Mian Singh. Katika kikao hicho baadhi ya mambo yalikuwa yanazungumzwa. Maulawii Ghulam Rasul aliyekuwa Walii na mwenye karama akiendelea kuongea akasema, "Kama katika zama hizi angekuwa nabii, basi huyu kijana anafaa kuwa nabii". Akasema hayo akipitisha mkono wake juu ya Hadhrat Masihi Mau'udi as. kwa mahaba. Maulawii Burhanud Din ra. anasema, mimi mwenyewe nilikuwepo katika kikao hicho." (Masimulizi ya Masahaba yasiyochapwa, Jl. 12, uk. 104, 105)

Masomo ya Seyyidna Ahmad as.

Kabla ya serikali ya Kiingereza, ulikuwepo utawala wa Masingasinga katika Panjab, na serekali ya Masingasinga haikujali elimu. Matajiri wa nchi walikuwa wakiajiri waalimu nyumbani mwao kama wakurufunzi. Mwanzoni mwa zama za Waingereza pia utaratibu huo uliendelea. Mpango huo huo ulifanyika kwa mafunzo ya Seyyidna Ahmad as. Kwa vile Hudhur ameeleza mwenyewe kuhusu mafunzo yake, kwa hiyo inaonekana vizuri kukariri maneno yake mwenyewe. Anasema:

Endelea uk. 2

Jamia Ahmadiyya Wagawa Zawadi ya Idi

Kwa fadhili za Allah na Baraka za Ukhalifa,Wanajamia Ahmadiyya walipata fursa ya kutekeleza maagizo ya Mtume Mtukufu s.a.w yasemayo, "furaha ya kweli ni lazima iwahusishe wasiojiweza", na "mtafuteni Allah katika watu wanyonge" kwa kugawa zawadi za Ei'd Mubarak kwa wasiojiweza.

Zoezi hilo lilifanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 21/05/2020 majira ya saa nne asubuhi mpaka saa sita mchana. Walengwa katika hafla hiyo fupi walikuwa kutoka katika mitaa mitatu inayozunguka chuo chetu cha Jamia,mitaa hiyo ni Msamvu B,Kitata na Ngerengere. Mchakato wa kuwapata na kuwafikia walengwa hao uliwahusisha viongozi wa mitaa hiyo na ndio waliowaongoza wananchi hao siku ya tukio hilo.Zawadi zilizotolewa zilikuwa ni kama vile Unga,Mchele,Sabuni nk. Tukio hilo liliripotiwa pia na vyombo mbalimbali vya habari kama vile Radio,Televisheni,magazeti nk.



Zawadi ya Idi mbele ya chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro tayari kufikishiwa walengwa.

Hafla hiyo ilifanyika katika viwanja vya Jamia kilichopo Kihonda Morogoro .Akielezea shabaha ya hafla hiyo ,Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib ,mkuu wa chuo chetu cha Jamia ambaye pia alikuwa ndiye mwenyeji wa shughuli hiyo,alisema, "Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya waislamu waahmadiyya ametuhimiza kuwahurumia ,kuwasaidia na kuwapenda wanadamu na viumbe wote kwa ujumla.Ni kwa kuzingatia hilo,zikawa zimebakia siku chache kabla ya kusherehekea siku kuu ya Ei'd ul fitr,tumeonelea

Endelea uk. 2

Hazina ya Mapenzi ni Khilafat Ahmadiyya uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kitabu Chako

Utoto na Masomo ya Seyidna Ahmad[as]

Kutoka uk. 1



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

"Nilipokuwa mwenye umri wa miaka 6 au 7, mwalimu mmoja wa lugha ya Kiajemi aliajiriwa kwa ajili yangu aliyenifundisha Kurani Tukufu na vitabu vichache vya Kiajemi. Mzee huyo aliitwa Fadhl Ilahi. Na umri wangu ulipofikia miaka 10 hivi, mwalimu mmoja wa lugha ya Kiarabu aliwekwa kunifunza, ambaye aliitwa Fadhl Ahmad. Nafikiri, kwa vile masomo yangu yalikuwa mwanzo wa kupanda mbegu ya fadhili ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo neno la kwanza la majina ya waalimu hao lilikuwa Fadhl. Maulawii huyo alikuwa mtu wa dini na mwema. Yeye alinifundisha vizuri na kwa bidii sana. Nikajifunza kwake baadhi ya vitabu vya sarufi na baadhi za kanuni za sintaksi. Baadaye nilipokuwa mwenye umri wa miaka 17 au 18, nilipata kusoma kutoka kwa sheikh mwingine aitwaye Gul Ali Shah. Huyo naye aliajiriwa na babangu hapa Qadian kunifundisha. Nikajifunza kutoka kwa bwana sheikh wa mwisho sintaksi, mantiki, utabibu na kadhalika nikajifunza elimu za kawaida za zama zile kadri Mungu Alivyotaka. Baadhi ya vitabu vya utabibu nilisoma kwa babangu, yeye alikuwa tabibu mahiri wa fani ya utabibu." (Kitabul Bariyya, uk. 140-150)

Katika dondoo hiyo, waalimu watatu waliotajwa. Miongoni mwao wa kwanza alikuwa Sheikh Fadhl Ilahi, mkazi wa Qadian, na alikuwa mfuasi wa dhehebu la Hanafii. Mwalimu wa pili, yaani Sheikh Fadhl Ahmad, alikuwa mkazi wa Ferozwala, wilaya ya Gujranwala, mfuasi wa dhehebu la Ahlul Hadith. Na mwalimu wa tatu alikuwa Sheikh Gul Ali Shah, mkazi wa Batala, na alikuwa Mshia. Ilmuradi, Mwenyezi Mungu Alipanga waalimu kwa mafunzo yake waliohusika na madhehebu maarufu ya Waislamu. Na ikawa hivyo kwa sababu hivi karibuni katika siku zijazo, yeye alikuwa apewe kazi kubwa ya kuwarekebisha Waislamu wote, na kwa mpango huo akajua kiasi fulani itikadi na matendo ya kila dhehebu kwa sababu ya walimu hao.

Muzaffardurrani@gmail.com

Jamia Ahmadiyya Wagawa Zawadi

Kutoka uk. 1

ni vyema tugawe zawadi kidogo kwa wahitaji ili nao waweze kufurahia siku kuu hiyo nah ii pia ni kutekeleza agizo la Mtume Mtukufu[saw] na maelekezo ya Khalifa wetu mpendwa[atba]".

Naye mwenyekiti wa mtaa wa Msamvu B mtaa ambao ndipo kilicho chuo chetu cha Jamia alisema, "Napenda nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru ndugu zetu kwa hiki wanachokifanya leo,hili ni jambo jema kua kuwakumbuka wasiojiweza katika mitaa yetu,Mungu awabariki sana." Aidha mwenyekiti huyo alitoa wito kwa taasisi zingine kuiga jambo zuri kama hili.

Kwa upande wake mwenyekiti wa mtaa wa Kitata akielezea tukio hilo alisema, "Tunaishukuru sana Jumuiya ya Ahmadiyya wanatusaidia sana kama hivi walivyofanya leo hii,na pia wanatusaidia upande wa afya,elimu,maji nk.Kama uonavyo wametuwekea kituo cha kuchotea maji,tunapata maji bure nk.Kwa kweli tunawashukuru sana ndugu zetu hawa waahmadiyya".

Ama kwa upande wa mwenyekiti wa mtaa wa Ngerengere alisema, "Kwa kweli tunawashukuru sana ndugu zetu Waahmadiyya kwa kuwasaidia wananchi wetu,maana tunao wahitaji wa aina mbalimbali kama vile wajane,yatima, waishio mazingira hatarishi na wengineo.Kwa msaada huu waliotupatia utawasaidia wahitaji wetu".



Kwa upande wa wanufaika hao ,nao walitoa shukrani zao kwa msaada huo na kuwaombea Mwenyezi Mungu watoaji na kuwaomba waendelee na moyo huo.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	**Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.**
Mhariri:	**Dr. Swaleh Kitabu Pazi**
Kompyuta:	**Ahmad Abdul Nasibu.**
Mchapishaji:	**Sheikh Bashart Ur Rehman**
Msambazaji:	**Mwl. Omari Ali Mnungu**
Wajumbe:	**1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga**
	2. Mahmood Hamsin Mubiru.
	3. Jamil Mwanga.
	4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Hadhrat Amman Jaan[ra]

Na Sheikh Abid Mahmood Butt
Jalsa Salana Tanzania 2019

Kutoka toleo Lililopita

Huruma Yake Kwa Viumbe.

Kama ilivyokuwa kwa mtume .s.a.w. kuonyesha huruma kwa viumbe vinginie ghairi ya wanadamu,Hivyo ndivyo alivyokuwa hadhrat amma jaan sahiba[ra] Hadhrat mirza shareef ahmad[ra] alipokuwa mdogo ambaye ni mtoto wake (hadhrat amma jaan[ra]) alikuwa anapenda sana kuwinda ndege akishirikiana na hakeem abdul – azizi sahib.

Ilitokea hivi kwamba siku moja katika mezi wa may hadhrat hakeem abdul – azizi sahib alimwambia hadhrat mirza shareef ahmad[ra] akachukue bunduki nyumbani ili wakawinde (ndege). Hadhrat amma jaan[ra] alikataa kumpa bunduki.Hakeem abdul – azizi sahib alipomwona hadhrat mirza shreef ahmad anakuja mikono mitupu, alifikiri kuwa huenda ni kwa sababu ya kuwa mtoto ndio maana hakupewa bunduki, Hivyo aliamua kwenda mwenyewe kuomba bunduki kutoka kwa hadhrat amma jaan sahiba[ra] Lakini HAZRAT AMMAN JAAN alikataa kutoa bunduki, akimwambia kuwa msimu huu ndege wanataga na kutotoa,Hivyo si vizuri kuwinda msimu huu, kama mtaenda kuwinda ina maana mtawauwa mama zao na kuwaacha watoto wao bila ya uangalizi wowote.Akaongeza kusema "mimi mwenyewe nina watoto na ninajua uchungu wake,kamwe sitaruhusu uwindaji wa ndege katika msimu huu (mwezi) huu.

Shauku Yake ya Kuchuma Thawabu

Hadhrat amma jaan[ra]alikuwa na hamu sana ya kuchuma thawabu kila alipopata nafasi.

Kwamfano tunaelezwa kuwa siku moja alikuwa anasali katika kile chumba maalum (baitul – dduaa) ambacho hadhrat masihl – mau'ud .a.s. alikitumia kwa kufanya maombi pembeni yake alikuwa amekaa mama mmoja,kutokana na joto kali mama huyo akawa anampepea kwa kutumia kifaa fulani.Hahdrat amma jaan[ra] alipomaliz kusali,naye mama huyo akaanza kusali,basin aye hadhrat amma jaan[ra] akachukua kifaa kile na kuanza kumpepea mama huyo.Hapo mama huyo akasali haraka haraka ili kumwondolea udhia hadhrat amma jaan.r.a. baada ya kutoa salamu, mama huyo akasema, je,wewe mheshimiwa unanifanyia hivi mimi nisiye na thamani yoyote? Hadhrat amma jaan.r.a.,akajibu kwa kusema,"je, na mimi nisifachume thawabu ?

Malezi Yake Kwa Watoto

Juu ya suala la malezi kwa watoto,mama huyu alikuwa mfano mwema na wa kuigwa,binti yake mkubwa aitwaye Hazrat Nawaab Mubark Begum sahiba[ra] akieleza juu ya hili,anasema "Nimeshawatazama watu wengi kuhusiana na desturi za malezi,lakini sikuwahi kumwona aliye m-bora kuliko Hazrat Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] katika malezi. Yeye hakwenda kusoma katika shule yoyote kwa ajili ya kupata ujuzi zaidi,alijifunza kidogokidogokusoma na kuandika kutoka nyumbani kwao. Lakini kwa kuona kanuni zake za malezi na tarbiyyat,inaweza kusemwa kwamba hii yote ni fadhili za Mwenyezi Mungu kupitia malezi aliyopata kutoka kwa Hazrat Masihil-mau'ud[as],yote alijifunza kutoka kwake.Kanuni yake ya kwanza ilikuwa ni kumjenga mtoto katika misingi ya imani,kuchukia uwongo kuwafundisha kuona haya(aibu)na kutokujali vitu vya kidunia kama vile pesa n.k.Hili lilikuwa ndilo somo lake la kwanza. Ndivyo alivyokuwa akituambia sisi tabia hii tuizalishe kwa watoto,kila kinachosemwa lazima akubali,bila shaka hata mtoto awe mtundu kiasi gani ,lakini anapokatazwa jambo mara moja aache,kama mzazi atamzowesha mtoto mapema kuwa kila amwambiapo jambo fulani anakubali.Basi kwa namna hii siku zote matumaini ya kurekebisha mtoto (watoto) yatakuwepo.

Ndivyo alivyokuwa akitufundisha,sisi hatukuweza kufikiria hata siku moja kuwa wazazi hawapo basi tufanye jambo wasilolipenda .Mama siku zote alituambia tusiseme uwongo.Na sisi tulijiepusha kabisa na uwongo,na sio kujiepusha tu bali tuliuchukia.Wala sijawahi kumwona hata siku moja mama amekasirika.Alikuwa akisema mtoto wa kwanza apewe malezi ya kutosha ,yeye ndiye atakuwa mfano wa kuigwa na wenzake watakaomfuata nyuma".

Naye Hazrat Mirza Nassir Ahmad r.h ambaye ni mjukuu wake na pia alikuwa Khalifa mtukufu wa tatu ,anasema:- "Hazrat Sayyida Nusrat Jahan Begum sahiba alikuwa akisema baada ya sala ya maghrib moja kwa moja kwenda ndani hakuna kwenda nje mtoto yeyote isipokuwa kwenye sala ya Isha.Utaratibu huu uliendelea mpaka tulipokuwa wakubwa. Hakuwa na tabia yakuongea kwa ukali.Siku moja aliwaita watoto kuja kula chakula alikuwa na desturi ya kutandika kitambaa chini na kuweka chakula na watoto walikaa wakila kwa pamoja.Mimi pia aliniita kuniambia kuleni nyote pamoja,kwa kuwa wakati huo umri wangu ulikuwa mdogo kulinganisha na wenzangu na kwa kuwa watoto hupenda kugombana wakati wa kula na kwa sababu ya kutofahamu,mimi nilikataa kwenda kula na wenzangu.Hapo Hazrat Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] badala ya kunikaripia,akaniambia kwa upole sana akasema,"haya usile chakula,lakini ujue hutapata chakula baadaye".Baada ya kukawia kidogo,nilijiunga na wenzangu nikala nao pamoja.Mbali na watoto wake,pia watoto wa wanajumuiya aliwapenda sana na aliwahesabu kama watoto wake .Alikuwa akiwatendea vizuri na hii iliwafanya wafurahi sana,alikuwa akiwasimulia hadithi za kuchekesha na kufurahisha.

Nasaha Zake Kuhusu Malezi Ya Watoto.

Juu ya malezzi ya watoto Hadhrat Amma Jaan[ra]. alihimiza kuwaamini watoto na ya kwamba wasemapo jambo lo lote tusiwaambie "unadanganya" au "unasema uongo" Akasema Hadhrat Amma Jaan[ra] "ukiona unamwamuru au unamtuma mtoto naye anatii bila ya kubisha basi ujue hapo umefaulu"

Yeye aliwarekebisha watoto bila ya kutumia ukali wala wao (watoto) kujisikia kufedheheka mbele ya wenzao.

Aliwafundisha watoto kuwaheshimu waalimu wao, inasimuliwa kwamba siku moja mke wa Hadhrat Sheikh Ya'qub Ally Irfan[ra] alikuja kumtembelea Hadhrat Amma Jaan[ra], wakati huo Hadhrat Mirza Bashirudin Mahmood Ahmad[ra] alikuwa bado mdogo na alikuwa ni mwanafunzi wa Sheikh Ya'qub Ally Irfani sahib[ra]. Basi ikatokea hivi kwamba Mian Mahmood[ra] alikuja na nyoka wa bandia (wa plastiki) na kumtupia (kumweka) karibu na mama huyo mgeni mke wa Irfani sahib[ra]., kama watoto wafanyavyo katika michezo yao. Mama huyo alishtuka na kuogopa sana, Hadhrat Amma Jaan[ra] akamtuliza mgeni wake na kisha akamwambia mtoto (Mia Mahmood[ra]) "nini hiki unamfanyia mke wa mwalim wako?" Hapo Mian Mahmood[ra] akakiri kosa lake na kuomba radhi.

Kuchukia Kwake Shirk

Hazrat Amma Jaan[ra] alichukia sana shirki na viashiria vyake vyote.

Inasimuliwa kuwa siku moja mama mmoja alimwambia Hazrat Amma Jaan[ra] ya kuwa ndugu yake aliugua sana na walihangaika sana kumtibu kwa kila njia lakini hakupona mpaka walipompa dawa fulani(akaitaja) ndipo akapona.

Hapo Hazrat Amma Jaan[ra] akasema kwa jazba "kwanini usiseme kuwa",tulipojaribu matibabu haya basi ikaonekana humo kulikuwa na matakwa ya Allah pia, ndipo ndugu yetu kwa fadhila zake akapona?".

Bila shaka tukio hili linatukumbusha ile kauli ya Hazrat Masihil Mau'd[as] isemayo "msitawakal juu ya dawa ,bali mtawakal juu ya Allah.

Katika tukio lingine inaelezwa kwamba,kulikuwa na mama mmoja ambaye alikuwa na redio yake,mama huyo alikuwa na kawaida ya kusiiliza taarifa ya habari za ulimwengu kila siku na baada ya kusikiliza taarifa ya habari,alikuwa anaenda kwa Hazrat Amma Jaan[ra] na kumweleza yaliyojiri kutoka sehemu mbalimbali za dunia.Siku moja mama huyo baada ya kusikiliza taarifa za habari,kama kawaida alienda kwa Hazrat Amma Jaan[ra] ili kumpasha habari za matukio ya ulimwengu kama alivyoyasikia redioni.Baada ya kumweleza yale aliyoyasikia ,akaongeza kusema "Namshhukuru aliyetengeneza redio kwa kazi yake nzuri na nijitolee kwake .Hapo Hazrat Amma Jaan[ra] akasema kwa ari kubwa ,"Nijitolee kwa Mwenyezi Mungu aliyejaalia akili mwanadamu ya kutengeneza vitu kama hivi.".

Bila shaka maneno haya ya Hazrat Amma Jaan[ra] yanatupa somo kubwasana,ambalo ni hili kuwa ,yawezekana mtu amiliki kitu kikubwa,kizuri na cha thamani kubwa,lakini kamwe asifikiri kuwa raslimali hiyo ni kwa sababu ya akili zake na nguvu zake, bali yupo Allah aliyemjaalia akili mtengenezaji aliyekitengeneza na akamjaalia na huyo mmiliki kuweza kukipata.

Nasaha za Hazrat Amma Jaan[ra]. kwa kina Mama.

Mwishowe ningependa kuweka mbele yenu baadhi za nasaha za hadhrat amman jaan[ra]. ambazo haswa zinawahusu wa kinamama. Nazo nitazifikisha mbele yenu kwa kupitia hotuba mojawapo ya hazrat khalifa tul masih wa tano[atba]

Hazrat Khalifatul Masih wa Tano a.t.b.a akizungumzia kuhusu nasaha za Hazrat Amma Jaan[ra]. katika Ijtema ya Lajna Imaa'illah Uingeraza alisema;

"Hivi sasa mimi ninaweka mbele yenu baadhi ya nasaha za Umm-ul-Mo'minin Hazrat Amma Jaan[ra]. ambazo alizompa binti yake mkubwa yeye na Hazrat Masih Ma'ud[as]. Hazrat Nawab Mubarka Begum saahiba wakati wa ndoa yake, nitataja baadhi ya mambo hayo."

Hazrat Amma Jaan[ra]. alisema; "usifanye kato jambo lo lote ukamficha mumeo au jingine lo lolote utakalolazimika kumficha mumeo, Mume hataona lakini Mwenyezi Mungu anaona. Na mwishowe jambo lile linadhihirika na kupoteza umuhimu wa mwanamke, anakosa hadhi na heshima yake."

Akasema tena "kama kuna jambo lo lote lililotendeka kinyume na ridhaa ya mume, usilifiche katu, liseme waziwazi, kufanya hivyo kuna heshima na kinyume chake katika kuficha kunaleta fedheha na kuaibika,na heshima ya mwanamke inashuka."

Akasema tena; "usizungumze pale mume anapokasirika, kama amemkasirikia mtoto au mtumishi nawe unajua kwamba mume hayuko shahihi katika kufanya hivyo, bali yupo katika hali ya kukasirika na anamkaripia mtoto ye yote au kumgombeza mwingine na unaona wazi kabisa kwamba yeye anafanya makosa, hata hivyo usizungumze mbele yake wakati huo."

Akaongeza zaidi; "mwanamke anayebishana na mume wakati wa hasira yake anakosa heshima. Mara nyingi magomvi yanatokea kwa sababu ya kukosa subira na uvumilivu kwamba wanarejesha majibu papo hapo na kuyafanyia magomvi yaendelee." Akasema; "katika hali hii ya hasira akikukaripia wewe kwa sababu ya kuingilia kati basi utafedheheka, baadae mume akishatulia ndipo itakuwa bora kumwambia kosa lake kwa upole kwa sababu kumrekibisha pia ni muhimu…"

Huzur a.t.b.a akaendelea kusema kwamba Hazrat Amma Jaan[ra]. alimsihi mtoto wake kwa maneno haya kwamba "ndugu na jamaa wa karibu wa mumeo na watoto wao uwachukulie kama ni wa kwako… usifikirie ubaya kwa ye yote, hata kama ye yote akikufanyia ubaya wewe uwatakie heri wote moyoni mwako. Kama ye yote akikufanyia ubaya mwache afanye lakini wewe moyoni mwako usiwaze ubaya kumhusu ye yote na hata kwa vitendo pia usilipize ubaya, kisha utaona Mweneyzi Mungu daima Atakujaalia heri."

Khalifa mtukufu[atba] anasema Hazrat Amma Jaan[ra]. mara nyingi alikuwa anawausia watoto wa-kike na kiume kwmaba, "wewe unaenda kwa wakwe, usije ukafanya jambo lo lote ambalo kwao moyoni mwao lisababishe chuki na bughdha, na liwe sababu ya fedheha kwako na kwa wazazi wako. Hivyo usiyaingilie masuala ya wakwe, mambo yao yanayoendelea yaache yaendelee. Wala usiwazungumzie mama mkwe na mawifi zako kwa sura ya malalamiko mbele ya mume wako."

(Hotuba ya Ijtemaa ya mwaka ya

Adamu: Nabii wa Kwanza Duniani, Si wa Kwanza Kuumbwa

Kutoka toleo lililopita

Na **Bw. Juma Iddy Abeid, Kigoma**

Heu tazama kitabu cha biblia juu ya suala la Adam kutokua wa kwanza kuumbwa pia. Kwa hakika waalimu wa biblia hawa kutofautiana na masheikh katika dhana hiyo ya Adam kuwa mtu wa kwanza kuumbwa.

Kama nilivyosema awali makundi yote hayo mawili yanafuata wazoweya waliyorithi toka zama za giza japo hawana ushahidi toshelezi wa kimfano. Waandishi wa kikristo wote wenye dhana ya Adam kuwa mtu wa kwanza kuumbwa, wao hujitia upofu kwa kujifanya sura ya kwanza ya kitabu cha mwanzo kuwa dibaji ya sura ya pili.

Hufanya hivyo kwa makusudi tu ili waende na kile wanacho amini. Jambo ambalo si sahihi. Na ukitazama sura hizo mbili kama zilizotenganishwa na wapangaji wa maandiko utagundua wazi kuwa Adam si mtu wa kwanza kuumbwa.

Mwanzo 1: 27-28 :- Mungu akaumba mtu wa mfano wake, kwa mfano wake alimuumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba.

Mwanzo 1: 28 :- Mungu akawabarikia Mungu akawaambia zaeni wakaongezeke makaijaze nchi na kuitisha, mkatawale samaki wa baharini na ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.

KUHUSU CHAKULA CHAO :- Mwanzo 1:29 :- Mungu akasema, tazama nimewapa kila mche utoao mbegu ulio juu ya uso wa nchi yote pia na kila mti ambao matunda yake yana mbegu vitakuwa ndivyo chakuka chenu.

Watu hao ni watu wa awali, kabla ya uumbwaji wa Nabii Adam, hao hawakupewa katazo lolote na jukumu walilopewa ilikuwa kuzaana kwa wingi ili kuijaza nchi watu hao wapo tofauti na Adamu na hasa watu walio kitabu cha :-

Mwanzo 2:7 :- MWANA MUNGU AKAMFANYA MTU KWA MAVUMBIYA ARDHI AKAMPULIZIA PUANI PUMZI YA UHAI, MTU AKAWA NAFSI HAI

AKAPANDA BUSTANI UPANDE WA MASHARIKI WA EDENI AKAMUWEKA NDANI YAKE CHAKULA CHAKE.

MWANZO 2: 16-17 :- Bwana Mungu akamuagiza huyo mtu akasema matunda ya kila mti wa bustani waweza kula walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile. Kwa maana siku mtakapo kula matunda ya mti huo utakufa hakika.

Bila shaka msomaji yeyote ambae hakuathiriwa na thiologia batili ataona wazi kuwa kuna watu wawili tofauti. Angalia watu wa kwanza Mungu aliwaumba watu wawili, mtu mume na mtu mke. Watu hao waliumbwa pamoja na hawakuwekwa bustanini. Lakini mtu wa pili kaumbwa mtu mmoja tu na akawekwa bustanini.

Pia kuhusu chakula watu wa kwanza hawakupewa pingamizi juu ya kipi wale kipi wasile. Wao waliambiwa MTI WOWOTE WENYE MATUNDA ITAKUWA CHAKULA CHAO. Hao ni tofauti na mtu wa pili yeye aliambiwa miti miwili asile mti mmoja ulikuwa wa mema na mabaya na mti wa pili mti wa uzima.

Katika kipindi hicho hicho kulikuwa na kundi lingine, kundi hilo lipo katika kitabu cha MWANZO 6:4 :- NAO WANEFILI WALIKUWAPO DUNIANI SIKU ZILE. Tena baada ya hayo wana wa Mungu walipoingia kwa binti za wanaAdam, wakazaa nao wana hao ndio walikuwa watu hodari zamani watu wenye sifa.

Kwa kweli mpaka hapo sidhani kama kunapingamizi dhidi ya uwepo wa watu kabla ya uwepo wa Adamu. Neno WANEFILI wamelifasili kwa maaana ya (majitu). Waandishi wa biblia wamesema kuwa majitu hayo yalikuwepo siku zile.

Isitoshe Adam alipokuwa na wana wawili wa kiume, mmoja alimuua mwenzake, na baada ya tukio hilo alipewa adhabu ya kuwa mtu asiye na makao duniani. Yeye atasema adhabu aliyopewa ni kubwa mno na watu wakimuona watamuua. Bwana akatangaza kuwa kumueke alama mtu yeyote asimuue MWANZO 4:12-15

Mafungu yote hayo yanaonyesha Adam alikuwa na watu mchanganyiko baada ya kufukuzwa bustanini, kwani bustanini alifukuzwa kwa kuhofiwa asije akala mti wa uzima na akaishi daima MWANZO 3:22-24

Katika tukio la mtoto wa Adam kuuwa yeye aliondoka eneo lile na kukimbilia nchi ya modi na huko alioa na akapata mtoto akamwita Enoko jina la mji ule. MWANZO 4: 16-17

Mpaka hapo bila kuongeza lolote inatosha kusema kuwa Adamu hakuwa wa kwanza bali ni mtu wa kwanza kupatiwa na Mungu juu ya mambo ya Imani ambayo yana ambatana na Muongozo.

Khalifa Wa Hizb-Ut-Tahrir Akwama Kwenye Vipimo: Unabii Unaendelea

Na **Bw. Hassan Sango**

Namshukuru sana Allah kwa fahili Zake Aliyetupatia dini ya Islam ambayo imekamilika.

Dini ambayo haikuacha jambo lolote la mwongozo isipokuwa imelieleza.

Ni muda mrefu umepita najadiliana na ndugu yangu Ntibarabara Moshi Kakoso kuhusu swala oa Ukhalifa na kuendelea Utume katika umati wa Mtume s.a.w.

Kuhusu suala la kuendelea au kutoendelea Utume, hakuwahi kunipa aya zaidi ya kuniambia Khatama maana yake ni mwisho bila maelezo zaidi.

Nilimfahamisha kuwa tunaomba tuongozwe njia iliyonyooka na njia hiyo mmoja wa wafasiri wa Quran Abdullah Yusufali ametoa maelezo ya Surat Fatiha kuwa kuongozwa huko ni kupata neema inayoelezwa katika aya inayofuata ambazo ni Unabii, ambao aliupata Mtume s.a.w., Usadiq aliupata Abubakar r.a., Ushahid waliupata Hassan na Hussein r.a., na Usalih huo ndio kundi kubwa la Waislam wamo sura 4:69 (Tafsir Abdullah YusufAli).

Kwa mantiki hiyo huyu mfasiri ameelewaa neno ma'a lililopo katika sura 4:79 (Tafsiri Abdullah Yusuph Ally)

Kwa mantiki hiyo huyu mfasiri amefasiri neno m'aa lililopo sura ya 4:79 Tafsiri yake hapo ni miongoni yaani kupata vyeo hivyo si kama wafikiriavyo baadhi ya watu kwamba ni kuwa pamoja tu bila kupata vyeo (alicchokosea yeye ni kitu kimoja kuwa wakati aya inashuka mtume s.a.w alikuwa kisha upata UNABII, lakini pia aya inasema atakaye mtii Mwwenyezi Mungu na Mtume basi hao ni miongoni mwa wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu Manabii na Masadiq na mashahid na masalih.

Mfamfasiri hapo juu ametoa tu mifano yaw t=atu waliopata vyeo hivyo, kwasababu vyeo vyote vipo katika wingi UNABII, USHAHIDI, USADIQ, MANABII, MASADIQ, MASHAHIDI NA MASALIH, hivyo ni wazi vyeo vvyote hivyo vitaendelea kupatikana katika umati wa Mtume Muhammad s.a.w. kadri atakavyopenda mungu

Tafuteni wenyewe tafsiri hiyo mujionee wenyewe maana Waahmadiyya wakitoa tafsiri sahihi masheikh aidha kwa maksudi au kwa kutojua wanasema wametoa tafsiri ili kumdaia utume huyo mtu wao.

Misikiti kadhaa hapa Dar es salaam nilizona tafsiri ihizo nunueni mujionee haki wenyewe bila kudanganywana hao wanodhani neema ya unabii katika uislam imeharamishwa

Niliwahi kumuulizaa ustadh mmoja kule Nguruka, Kigoma hivi waislam wakifanya maovu kama nyimati zilizopita kabla yao wataadhibiwa kama wao? Ustadhi haraka alijibu kwanini wasiadhiwe wakati wamefanya kosa? Swali langu la pili lilimpa wakati mgumu sana je? Wakifanya wema watalipwa kama watu wa zamani? Akona sasa swala la unabii linakkuja.

Hawa ndio waelezao habari za nyoka na nge kaburini na kupigwa nyundo kila wakati wa swala ukifika kama ulikuwa huwali, lakini neema za kiroho zipatikanazo katika Islam wanaona aibu kuzitaja.

Hawa ndio wasemao kuwa waislamu watakuwa pamoja na watu walioneemeshwa MASADICK huko peponi lakini wakienda msikitini siku ya ijumaa kwa sauti kubwa kabisa wanatangaza Amirukk Muuminin Abubakar Swidiq na maamuma wanaitikia kwa kuwa Sadiq radhi ya mungu iwe juu yake . kweli muongo hana kumbukumbu anajipinga mwenyewe

Wakisema Ahmadiyya UNABII, USADIK, unaoatikana katika ummati wa mtume s.a.w wanaambiwa tafriri tafsriri ili kumdaia utume mtu wao.

Sasa ustsdhi mbona unaenda msikitini siku ya ijumaa unatanga kwenye hotuba Abubakar kaupata usadiq na sio tu atakuwa pamoja na Masadiq huko peponi.

Tena wakati anatangaza hivyo sio kama kuna Ahmadiyya labda kashika panga anakutisha lahasha!

Sasa imam anappindua tafsiri kama Ahmadiyya yeye anataka nini?

Hivi unatimiza usemi wa kiha, byo mwanka nibiyo muhiya yaani vile mnav yaani vile mnavyovikataa vile mnavyovikataa ndivyo mnavyovila mwenye masikio na asikie

Sasa turejee katika ukhalifa ambao watu wa hizo tafsiri wanadhani kuna ujanja aw kuweza kuupata

Tangu zamani suala la vipimo lina umuhimu mkubwa katika masuala mbalimbali

Mda mrefu umepita najadiliana na ntubabara kakoso kuhusu kuendelea kwa utume na ukhalifa

Ni kwenye 28/11/2019 nilipoamua rasmi kumtumia kipimo kilichowekwa na mtukufu mtume s.a.w. juu ya upatikanaji wa ukhalifa baada yakekwa kuotia simu ya mkononi nilimuandikia hadithi ifuatayo "UNABII UTAKUWA KATI YENU PAKA APENDAVYO MWENYEZI MUNGU, KISHA UTAPATIKANA UKHALIFA JUU YA NJIA YA UNABII NAO UTAENDELEA PAKA ATAKAPOPENDA MWENYEZI MUNGU, KSHA UTAPATIKANA UTAWALA WA MABAVU NA KISHA UTAPATIKANA UKHALIFA JUU YA NJIA YA UNABII, ndipo Mtume s.a.w akanyamaza (mishkat kitabul fitan)

Chini ya hadithi niliweka maswali yafuatayo

Huo ukhalifa hizb ut tahirir unapatikana kwa njia ipi na unabii mumeufunga?

Jibu la ntibara kakoso ukhalifa unaotakiwa ni uanoelezwa na hizb ut tahirir sio huo mnaoufahamu nyie makadian.

Wasomaji watukufu maswali niliyouliza yamejibiwa?

Lakini siku zote na NTABARA wa hizb ut tahirir zaidi ya miaka 20 sikuwahi kusikia amanita kadian, sasa sijua aliamua kuniita hivyo kutokana na uzito wa maswali

Lakini ndugu huyo hakuishia hapoana niilumu kuwa ufahamu wangu mdogo sielewi majibu yake, ndio maana ndio maana nimeleta kwenu wasomaji watukufu muone nani anasifa hiyo

Swali lingine nililouiza nipatie kutoka katika historia watu walipokosa ukahlifa walikuwa wanapita huku na huko kufanya

Inaendelea uk. 5

Khalifa Wa Hizb-Ut-Tahrir Akwama Kwenye Vipimo

Kutoka uk. 4

vikao na kuhamasisha wakapata Khalifa

Kama kawaida akatoa jibu ambalo haliendani na swali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mtoaji wa riziki lakini sisi huitafuuta wenyewe

Kwa hakika jibu hilo laweza kumdhihirisa asiyejua ni tofauti kabisa

Jubu langu Mungu hajaeleza njia maalumu ya kupata riziki bali alichoeleza ni kupata ya halali

Hajsema upate kwa uvunaji asali au uvuvi

Lakini Ukhalifa mungu kaeleza njia ya kuupata

Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vuzuri bila shaka atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea na atawabadilishia Amani baada ya hofu yao. Wataniabadu, hawatanishirikisha na chochote na atakaye kufuru baada ya hayo basi hao ndio wavunjao amri sura ya 24:56

Hapo tumeona njia ya kupata ukhalifa ahadi ya Mungu kwa malioamini na kufanya vitendo vizuri, pia Mungu kaeleza watakuwa kama wa kabla yao

Kuwa zamani baada ya manabii kufariki walipatikana makhalifa

Wakati aya ya Qur'an ikieleza hivyo mtume ameeleza uaptikanaji wa ukhalifa katika umma wake kama tulivyoona katika misakaati kibul-fitan

Pia mtukufu mtume s.a.w anaeleza aneleza zaidi anasema wale waliobaki nyuma yangu watashuhudia machafuko makubwa na vurumai nasaha yangu kubwa uwa mtembee katika nyayo zangu na nyayo za makhalifa walioongoka watokanao na makhalifa karibu ya muda wangu. Hao watakaoongozwa kwanjia sawasawa ni lazima muwafuate kwa uaminifu kabisa kwa uaminifu na kwa kufunga maana nao kwa umadhubutu kama vile mtu anavyoshukulia kwa nguvu sana kwa meno yake. Na kamwe msiachane na suna zangu na suna za makhalifa walioongoka (musnad ahmad bin hambal jalada la 4 uk 127

Baada ya kuona kalifa wake mtarajiwa hana nafasi katika vipimo vilivyotolewa na mtukufu mtume s.a.w badala ya kumlaumu Mtume kwa nini kaweka vipimo hivyo

Akaamua kumrukia mtu alidhani kuwa ni mnyonge aakanitumia meseji akanitumia meseji safari hii anaita sheikh manukuu

Sikia sheikh hasani, Ahmadiyya kuanzishwa kwake ilikuwa kuja kuwachanganya waislam na kuwavuruga ili wapoteze lengo waliokuwa nalo la kuwafanya juhudi za kurudisha utawala wa kiislam kihalal urudi tena na watu wahukumiwe na sharia za Allah

Baada ya kuwa Mustapha Kamal at turuke kafir huyu kwa kushirikiana na waingereza khatimaye khalifa kuondoshwa

Ndipo muingereza akaplan mpango wa kutangaza mtume mwengine kapatikana ili wapambane nalo na waachane na jambo muhimu ndipo sasa aktokea Mirza. Mwisho wa kunukuu

Waswahili walisema kweli chiruku mzee hakamtwi na makapi

Kwanza kabisa kutokana na maneno hayo inaonyesha tamaa za ukhalifa wa kihizo ut-tahirir wamempofusha hata asiweze kuelewa maana maana ya hadithi ya mtume s.a.w iliyopo mishakti kitabul fitan kuwautme utakuwepo mpaka atakapopenda Menyezi Mungu, kisha utatikanaukahlifa juu juu ya njia ya unabii nao utaendelea mpaka atakapopenda Mwenyezi Mungu KISHA ATAPATIKANA UTAWALA WA MABAV, katika sehemu hii ndio unapatikana huo yeye unaouita khilafat

Hivyo waingereza kama ni kweli basi watakuwa waliodondosha utawa ulikuwa unaendeshwa na waislam wakiwa kiongozi wao wameshamuita Khalifa

Na si khalifa sawa hadithi ya mtume s.a.w ambayo ndugu yangu alitoroka kujibu maswali yangu

Lakini hawa ndugu zetu kama kawaida yao bila kuleta ushahidi huyu bw. Mustapher at turuke kafiri hii tunawaachia nwenyewe.

Kwa mujibu waa Mtume s.a.w huwezi kudai ukhalifa lazima kwanza uthibitishe unabii kwa kule kwetu kigoma huwezi kufyeka michikichi halafu ukategemee utaona michikichi sasa ndugu yangu anafyeka unabii halafu anataka uone ukhalifa ajabu, kwa mujibu mtume KISHA UTAPATIKANA NA UKHALIFA KWA NJIA YA UNABII wasomaji watukufu mnaweza wenyewe kuona jinsi jinsi gani bwana mwenye ufahamu mkubwa lakini haielewi au amefanya ubahili hataki kutumia ufahamu wake kwa ukweli unaoelezwa na kudhani basi kama anafanya hivyo ajue anakiuka agizo la mtume s.a.w aliyesema, 'kila jambo la hekima ni mali ya muumini iliyopotea popote atakapoiona aichukue'

Kwa hayo tumeona kwa hakika mtu afanyaye mpango eti upate khalifa bila kupitia unabii mtu huyo anakiuka nasaha za mtume (s.a.w) alitufahamisha hutokea kwa njia ya unabii si vinginevyo aliyesema LAZIMA UKHALIFA UPATIKANE KATIKA UMATI WAKE KWA NJIA YA UNABII SI VINGINEVYO

Kwa masikitiko makubwa eti Mirza alitumiwa na waingereza kuwavuruga waislam (mungu apishie mbali dhana hii) wasishughulikie ukhalifa.

Tumekwisha ona sawa na hadithi ya mtume (s.a.w) ukhalifa usingeweza kupatikana bila unabii.

Seyyidna Ahmad a.s (mirza) asingeweza kutumiwa na waingereza wakati mkononi mwake alikuwa bunduki (hoja) inayomwua nabii issa (a.s) ambaye wao wanaamini ni mungu mwana na yuko mbinguni.

Lakini kama Ntibabara angekuwa ni mwenye bahati ya kutafakari angejiuliza kama kule india ni mirza kadhoofisha uislam huku kwingineko nani kadhoofisha , ni kweli uislam umedhoofika baada ya madai ya unabii wa mirza au kabla? Huo awadhani ni ukhalifa huku kwetu ulisaidia nini?

Enyi mlioamini! Mtiini mwenyezi mungu na mtiini mtume wake na wale wenye mamlaka miongoni juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lolote , basi lirudisheni kwa Mwenyezi Munguna Mtume, ikiwa ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na siku za mwisho. Hiyo ndiyo heri nayo inamatokeo bora

Maelezo yanayotulewa na Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya ni kuwa muundo wa lugha za kiarabu wa fungu la maneno uulil amir muukum (wenye mamlaka) haujaeleweka sawasawa na na baadhi ya watu. Na lenye utashi maalum ni neno minkumambalo kwa hakika linaundwa na viarifu viwili vilivyounganishwa pamoja yaani min na kum min maana yake ni kutoka na kum maana yake ni ninyi. Kwa kulitafsiri kwa mtindo wa neno kwa neno, baadhi ya mufasirina walielewa fungu hili la maneno kuwa na maana ya kutoka miongoni mwenu, yaani mnatakiwa kuitii ile mamlaka ambayo inabahatika kuwa kutoka miongoni mwenu, ikiwa na maana ya mamlaka ya kiislam peke yake. Katika mfano huu maalum hiki kiarifu min kinafanya kazi ya kuunganisha kile kiarifu kum na lile nino ilil amri katika uhusiano wa kumiliki na tafsiri ni lazima iwe wale wenye mamlaka juu yenu.

Katika maana iliyopanuka zaidi ya maneno hayo wanawakusanya hata wale wasio waislam. Sunna na hadithi za Mtume s.a.w. zimeweka wazi jambo hili ya kuwa katika mabo ya kidunia waislam wawatii hata hao watawala wasiokuwa waislam kama hawaingii kuvuruga taratibu za dini zao

Chini ya aya hiyo Sheikh Abdallah Saleh Farsiy ameandikia kilamwenye kutawalishwa inataka watiiwe maadam wanayoamrisha ndiyo ndivyo.

Ikiwa hapana mkubwa wa kutiiwa yatakuwa mambo hovyohovyo na itakuwa fujo. Na uislama haupendi mambo ya ovyoovyo wala dhuluma na ujeur

Katika maelezo ya aya hiyo A Yusuph Alli 1934 imetolewa huyu sio Ahmadiyya ameandika ifuatavyo:-

Ulil-amri those charge with authority or responsibility or decision or the settlement of affairs. All ultimate authority rest in God. Men of God derive their authority from him. As Islam makes no sharp division between sacred and secular affairs. It expert ordinary governments to be imbued with righteousness and stand in the place of righteous iman. And we must respect and obey such authority. Other wise there will be no order or discipline where in actual fact, there is the morality between secular and religious affairs, as is the case in most countries at the present day. Islam still expect secular authority to be exercised in righteousness on the condition. Enjoins obedience to such authority.

TAFSIRI:.....

Wakati huyu bwana akitoa mnaelezo haya 1934 india na pakistan ilikuwa nchi moja na utawala ulikuwa chini ya wasiokuwa waislamu wahindu.

Bw. Ntibara kaiulizia sana kuhusu aya hiyo akidhani kuwa waislam hawatakiwi kuwatii watawala wasiokuwa waislam ili kutetea anaedhani ni Khalifa ashike dola.

Islam biula shaka ni dini iliyokusudiwa kuondoa matatizo ya dunia kwa kuyapatia ufumbuzi, lakini kwa bahati mbaya hawa waislam wasioelewa wameongeza matatizo yao wenyewe na ya Dunia kwa ujumla

Aya nyingine imsumbuayo ni 51 sura al-maaida: je? Wao wanamtaka hukumu ya siku za ujinga? Na nani aliye mwema zaidi kuliko Mwenyezi Mungu katika hukumu na watu wenye yakini? (tafsiri ya Ahmadiyya). Sheikh farsiy: je? Wanataka hukumu za kijahili (ya zile siku za ujinga kabla ya kuletwa mtume) nani aliyemwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini.

Aya ipo wazi wala haikatazi kutii serikali isiyokuwa ya kiislam kama alivyodhani ndugu yangu

Dai lake lingine ni kuwa Mirza alikuwa masikini njaa mpaka kichwani, sijui kapata wapi habari hizi?

Lakini uislam haukatazi mtu masikini kuwa nabii 93:9 na akakukuta mhitaji naye akakutajirisha?

Bahati mbaya hawa hawasimi qur'an bali wao wanataka tu Khalifa wao kamate dola na kuongoza kiislam wakati hawana habari na Qur'an sasa sijui Islam wataipata wapi?

Jambo lingine ni kuwa Khalifa wa tano wa Ahmadiyya ni mshirikina (mungu apishe mbali dhana hii) kwa kuwa katika kipeperushi. Khalifa mtukufu V*atba* alisema kuna kundi kubwa la waislam wasio nchi za magharibi na karibu ni kila sehemu ya dunia.

Waislam ni wapili kwa nguvu kubwa na idadi ya watu hata kidini, katika ulaya waturuki ni mamilioni

Na makundi mengine ya waislam toka Asia wanahamia UK, USA, Canada, na karibu na kila nchi ya ulaya.

...

kwa hakika ushauri huo ndio ufaao kwa kukomesha hali ya kudhihakiwa watu watakatifu na maelezo hayo hayana chembe ya ushirikina.

Lakini pia ilitakiwa atoe njia aonayo inafaa sawa na mafundisho ya Islamsababu ameruhusu upigaji kura wa kidemokrasia.

Wakati demokrasia ni haramu nilimuuliza uharamu wake uko wapi hakujibu.

Itaendelea toleo lijalo

Bustani ya Washairi

HADAA ZA WANAWAKE

1. Yahitaji umakini, na subira nyingi sana
Hata kama una dini, kukosa Sala hakuna
Ni maua ya chumbani, ila 'siamini sana
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

2. Ila 'siamini sana, hata wale wa shambani
Kugusana ni hapana, utazama maungoni
Hata kama wamenona, siwatazame machoni
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

3. Siwatazame machoni, dhambi utazitafuna
Tuwaweke migongoni, ili tusiweze ona
Nawakumbusha jamani, wala siongei sana
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

4. Eti kuna urafiki, mwanaume mwanamke
Tusilete unafiki, tusijepata maseke
Mungu tusimdhihaki, sicheze na mwakamke
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

5. Sicheze na mwanamke, hata kama una laki
Atakufanya Bushoke, hatakama hautaki
Waulize wa Temeke, wanatembezwa mswaki
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

6. Usilete itifaki, kwa mambo wa wanawake
Wewe jifanye konki, huko ndani wakusweke
Kule hupatikaniki, huku mefanywa udeke
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

7. Kuwa makini kijana, duniani mitihani
Usipige dana dana, ukaribie ndoani
Uache kugandamana, na sumu za kiunoni
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

8. Hawa viumbe jamani, wala 'sishindanenao
Silete upunguani, na watu wa muambao
Utabebwa mgongoni, takua kalagabao
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

9. Huyu huyu mwanamke, ishi nae kwa akili
Ni lazima mkumbuke, wana mioyo miwili
Ngoja siku acharuke, utaona mbili mbili
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

10. Ila kwa ufupi sana, usiwaamini kamwe
Ukiona sina mana, tafakari kwali mmwe
Kwa nyakati za mchana, hawapendagi watumwe
Hadaa za wanawake, kusumbua wanaume.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
Kalindimasenior@gmail.com

TOA

1. Hiyo mali ulochuma, kuna siku itatoka
Wakati bado mzima, au ukipukutika
Waza sasa la kupima, jinsi itakavyotoka
Utoe wewe mwenyewe, au watoe wengine.

2. Kutoa ni taadhima, toa upate Baraka
Toa bado una hema, pasi nguvu kutoweka
Hiyo kabiri neema, Anafurahi Rabuka
Lakini usipotoa, wataitoa wenzio

3. Toa upate ghanima, ni akiba umeweka
Siku ile ya kuzama, mlingoti utashika
Upate vuka salama , hadi bandari kufika
Nayo bandari salama, Firidausi naima.

Mahmood Hmasin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

HOFU YETU MOLA WETU

1. Dunia yote gizani, Zimefugwa njia zote
Mawazo karantini, Hofu ipo pote pote
Ulimwengu hatarini,Kufutika tuokote
Wewe ndio kimbilio, Mola wetu tunusuru

2. Janga juu ya majanga, Ila hili ni Kisanga
Wenye mitaji ya kanga, Machinga kutangatanga
Hakuna pa kuzichanga, Huu wa shingo upanga
Masharti tunafwata, Mola wetu tunusuru

3. Tumrejeeni Karima, Na dua ndo suluhisho
Amimine takrima, Atukinge na vitisho
Tii Khalifa wa zama, Hili langu hitimisho
Hofu yetu Mola wetu, Mengineyo yakupita

Shabani A. Shunda
Shunda Mshundia Wana
Daluni Tanga
+2556565577321

KENGE KAVAMIA KAYA

1. Yailahi ya latifu, Mola mkinga machafu
Mola ulojaa shufu, Uwezo wako khalifu
Dunia yetu hafifu, Wawajua wahalifu
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki

2. Kila mahala ni hofu, Taharuki duniani
Kenge mwenye masharafu, Kaingia na nchini
Analeta usumbufu, kwa waja wa Manani
Kenge kavamia kaya, Taharuki duniani

3. Amejawa na mafua, Katokea uchinani
Kwa homa ana lembua, Machozi hadi puani
Kikohozi ndiyo fani, Wazee ni taabani
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki

4. Kenge hachagui mtu, Anaingia mwilini
Kinga yako iwe kuntu, isiwe ya ukingoni
Wale walopata kutu, Afya yao mashakani
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki

5. Mikono mkishikana, Yeye anafurahia
Na tena mtapatana, Abaki kushangilia
Na Mkikumbatiana, mvinyo ajimwagia
Kenge kavamia kaya, Abaki kushangilia

6. Kenge si mgeni sana, Alipata kufikia
Habari hii ni pana, Wengi wasioijua
Aliondoka mchana, Jua likimuwakia
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki

7. Kwa maadui maradhi, huyu kenge hana hadhi
Tena awatake radhi, China walimhifadhi
Kwetu Sala ni faradhi, Mara tano kutawatadhi
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki

8. Beti nane iwe somo, Kenge aende mchomo
Dini iwe ni kipimo, Arudi kwenye mashimo
Tena iwe ni kikomo, Tuushike msimamo
Kenge kavamia kaya, Nyumba zinataharuki.

Mazongera Pazi

HATIMA

Hatima iliye njema, maombi ninakuomba
Nakuomba ya Karima, Rabi Aliyeniumba
Uwe mwisho wa ghanima, wa Imani isoyumba
Na safari ikifika, nije kwa kuheshimika.

Mahmood Hamsini Mubiru (Wa Mamba)
Bukoba - Uswahilini

KWA HERI NI WETU BWANA

Ramadhani wetu bwana, kwa wema uliingia
Nasi tulishikamana, kwa wema kukupokea
Tlifunga kwa dhamana, kwa fadhila za Jalia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Nyoyo zilitakasika, kwa kuzileta fadhila
Na mbaya alidhikika, kimya akamba kulala
Shetani ni msifika, kwa ubaya wa mikwala
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Ulimwengu hutulia, ukakunywa kama tao
Wa hii yetu dunia, yalisha majaribio
Kila mja alilia, na kumsaka kwa mbio
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Usiku tulisimama, Manani kumlilia
Tulikimwomba Karima, mema kutuzidishia
Mabaya yapate koma, sote tupate tulia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Ramadhani mtajika, karibu tena mwakani
Mola wetu Msifika, Atujalie mwakani
Tufikie kwa hakika, tuyapate ya Manani
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Shukurani nazitoa, kunijalia kufunga
Kwake nikaelekea, kaongeza wake mwanga
Wemawe kanitolea, na mabaya kunikinga
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Kaditama nimefika, sio mwisho wa kuomba
Uyaondoe mashaka, tupate nyoyo kuwamba
Utulivu kuuweka, kama ngozi yake mamba
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Harun R. Bundala
S.L.P. 54, Tabora

MKE BORA.

Ya rabbi Mola karimu, Mjuzi wa Kila Kitu,
Mja ulonikarimu, Leo nakuomba Kitu,
Tena chenye umuhimu, Chenye tija hicho Kitu,
Nijalie Mke bora, Mke mwenye siha njema.

Dini yako Takatifu, kwa Mjumbe ulotuma,
Kafundisha yakinifu, Na mema yote kusema,
Ukioa umekifu, kwa Imani yote njema,
Nijalie mke bora, Mke mwenye siha njema.

Awe Mzuri wa Sura, Mwenye kuipenda Dini,
Unifanyie nusura, Asiichukie Dini,
Awe na tabia bora, Asidharau wa chini,
Nijalie mke bora, Mke mwenye siha njema.

Awapende ndugu zangu, Asiwe mwenye majungu,
Atii wazazi wangu, Tena awe Mchamungu,
Yeye ndiye ndoto yangu, Laliapo bavu wangu,
Nijalie mke bora, Mke mwenye siha njema.

Na mwisho yanilazimu, Kuomba kwako karimu,
`Sinipe mwendawazimu, `Siyejua umuhimu,
Nikaja kukulaumu, Mola wangu Mkarimu,
Nijalie mke bora, Mke mwenye siha njema.

Abubakary Abdallah Mwita. (Mkurya halisi.)

Ulimi na Moyo



Luqmān alikuwa ni Mtumwa kutoka nchi ya Ethiopia ambaye alikuwa ni Seremala.

Bosi wake alimwambia:
"Tuchinjie Kondoo huyu," basi akamchinja Kondoo.

Bosi wake akasema kumwambia Luqman: "Tuletee vipande viwili vilivyo Vizuri kutoka kwa Kondoo huyo," basi Luqman akampelekea Bosi wake Ulimi na Moyo wa Kondoo.

Kisha ukapita muda, vile alivyokadiria Allāh, na Bosi wake akamwambia tena Luqman: "Tuchinjie Kondoo huyu," basi akamchinja.

Bosi wake akasema: "Tuletee vipande viwili ambavyo ni Vibaya kutoka kwa Kondoo huyo," basi akampelekea Bosi wake Ulimi na Moyo wa kondoo.

Bosi wake akasema kumwambia Luqman: "Nilikuambia uniletee vipande viwili Vizuri, na ulinileta hivi (Ulimi na Moyo), kisha nilikuambia uniletee vipande viwili Vibaya, na ulinileta tena hivi hivi (Ulimi na Moyo)!"

Luqmān akasema: "Hakuna Viungo vilivyokuwa Bora kuliko hivi ikiwa hivi ni Vizuri, na hakuna Viungo vilivyokuwa Vibaya kuliko hivi ikiwa hivi ni Vibaya."

Tafsir ibn Kathir 12/31.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 20 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

F	F	U	T	U	R	U	N	B	L	D	B	Q	L	Q
T	T	W	E	M	A	M	N	Z	U	T	Z	X	P	D
T	V	A	Q	F	K	M	A	K	H	W	H	K	N	G
F	F	T	R	N	W	F	A	U	X	N	M	I	R	T
S	L	K	L	A	L	D	N	M	U	D	K	H	J	I
H	Y	B	N	A	W	P	Z	T	M	D	T	M	B	A
A	S	A	U	M	U	E	T	A	Q	W	A	M	T	B
W	M	I	F	M	K	L	H	V	B	Q	A	P	R	N
W	A	X	H	Y	R	F	H	S	H	H	V	T	A	L
A	O	M	Y	R	T	L	A	I	D	X	Q	R	M	Z
L	M	A	B	D	X	L	L	S	L	J	U	R	A	B
V	B	S	W	K	H	S	V	Q	I	Q	Y	W	D	D
C	I	I	N	K	U	B	H	X	R	K	J	Y	H	Q
Q	K	H	I	M	K	H	G	X	J	T	I	C	A	M
J	L	I	X	N	M	W	A	M	I	N	I	O	N	H

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Vileja Vya Chocolate na Vanilla

Na **Mtandao**



Mahitaji ya Kupika Vileja vya Chocolate na Vanilla

- Unga wa ngano vikombe 3
- Baking soda 1/2 kijiko cha chai
- Chumvi 1/4 kijiko cha chai
- Siagi kikombe 1
- Sukari nyeupe vikombe 2
- Mayai 2, yalopigwa
- Vanilla kijiko 1 cha chai
- Unga wa cocoa (cocoa powder) 1/4 kikombe

Jinsi ya Kupika Vileja vya Chocolate na Vanilla

1. Changanya unga pamoja na baking soda na chumvi. Weka pembeni.

2. Piga siagi na sukari kwa kutumia mchapo au mwiko hadi mchanganyiko uwe mweupe

3. Tia mayai na vanilla kisha piga tena vizuri kuchanganya.

4. Tia unga kidogo kidogo ukiwa wachanganya hadi ujikusanye na kufanya donge, gawa nusu kwa nusu

5. Katika donge moja tia kokoa (choco primo) kisha changanya vizuri upate donge la chocolate

6. Sukuma donge lako la vanilla kufanya umbo pembe nne, weka pembeni, kisha sukuma donge lako la chocolate umbo pembe nne pia. (kama unga unakusumbua unalainika tia katika jokofu (friji) kwa muda wa nusu saa kisha sukuma)

7. Bebanisha zote mbili ukianza na wa vanilla chini wa chocolate juu kisha sokota (kama wakunja busati) kisha zungusha katika plastiki na tia katika friji hadi uwe set mgumu.

8. Washa oven joto 180°C. Funika trei lako la kuokea kwa karatasi ya kuokea au zungusha kwa foil. (unaweza pia paka tray yako mafuta kisha nyunyiza unga)

9. Toa unga wako katika friji kisha kata vipande kwa kutumia kisu kikali, Panga katika trei na hakikisha unaacha nafasi kila baada ya kimoja.

10. Weka kwa muda wa dk 10-15 ziwe set vizuri na kupata rangi pembezoni na chini kwa mbali.

11. Epua kisha wacha zipoe kabisa katik trei.

Jinsi ya Kusafisha Mafuta



Jinsi ya kusafisha mafuta mfano uliyokaangia samaki.

⇢ Yachemshe.

⇢ Yakishachemka chukua limaoa au ndimu kata kipande.

⇢ Kitumbukize humo uchafuu utapanda juu.

⇢ Utoe yakipoa yanakua meupeee na hayana harufu.

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Ahueni ya Hatari Zinazotuzunguka

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

Ni karibu mbingu zipasuke toka juu yao, na Malaika hutukuza kwa kumsifu Mola wao na huwaombea msamaha waliomo ardhini. Angalieni! hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. Surah 42:6

MBINGU ni Paa 2:23 na Paa huangalia vyema athari mbaya za mazingira na kustawisha maendeleo mbalimbali. Mazingira yanaharibiwa basi Paa huharibika katika mazingira kama hayo ufanisi wa Paa huondoka. Manufaa ya mbingu huondoka na kusalia Fadhili na Rehema za Allah moja kwa moja. Rehema ya vitu vilivyofanywa Rehema inapoondoka, Rehema inayobakia ni Rehema ya Allah ya moja kwa moja isiyopitia kwa vitu.

Rehema hii ni Kubwa na ndio hunusuri vitu vyote vinavyozungukwa na Hatari. Anguko, ajari, maafa, ugomvi, hitilafu hutokea ikiwa Rehema ya Allah ikikosekana.

Aya hii imeeleza namna tatu ambazo zikitumika au zinavyotumiwa huwezesha kuwepo kwa Nusura ya shida zote;

1. Kumtukuza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu. Kumtukuza Allah kulimuokoa Nabii Yunus a.s asibaki kwenye tumbo la Samaki 37:140-144

2. Kuombea msamaha waliomo ardhini. Ndio njia ya Rehema 71:11-13

3. Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. Ambao hawafanyi makosa hali wa wakijua 3:136-137 hali hii imeendelea kuinusuru dunia na watu wake. Makosa mengi ni ya ujinga au kusababishiwa hivyo huruma ya Allah huwakumba.

Imeandaliwa na Musa Salum 0717504690

Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri. Amin

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

"Msidhani kwamba Mungu atawaacheni mteketee, nyinyi ni mbegu ya mkono wa Mungu iliyopandwa ardhini. Mungu Anasema, mbegu hii itakuwa na kustawi na matawi yake yata tokeza kila upande na itakuwa mti mkubwa. Hivyo amebarikiwa yule aaminiye Neno la Mungu na asihofu majaribio yajayo njiani, kwa sababu kuja kwa majaribio ni jambo la lazima ili Mungu Awajaribuni kwamba ni nani aliye mkweli katika madai yake ya kufanya baiati na ni nani aliye mwongo. Yule atakaye teleza katika jaribio lolote lile huyo hatamtia Mungu hasara, na bahati mbaya itamfikia hadi motoni. Ingekuwa vyema kwake kama asingezaliwa.

Lakini watu wote wale watakaofanya subira hadi mwishoni na mitetemo ya madhara itawakumba na tufani za taabu zitawavumia na kaumu zitawacheka na kuwadhihaki na dunia itawatendea kwa chuki mno, hao hatimaye watakuwa ni wenye kushinda na milango ya baraka itawafungukia. Mungu Ameniambia kwamba niiambie Jumuiya yangu kuwa wale watu walioamini, imani ambayo haikuchanganyika na dunia wala haikuchafulika na unafiki au woga, na imani hiyo haijakosa kiwango chochote kile cha utii, watu wa aina hiyo ni wapendwa wa Mungu, na Mungu Anasema kwamba ni hao hao ambao hatua yao ndio hatua ya kweli."

(Risala Al Wasiyyat, Roohani Khazain Jal. 20, uk 309)

MATUKIO KATIKA PICHA

1



2



3



4



1, 2, 3, 4 - Ukarabati wa vifaa vya sola na MTA ukiendelea katika mikoa ambapo vilileta hitilafu.

5



6



7



5, 6, 7, - Maadhimisho ya Siku ya Ukhalifa tawi la Jamia Ahmadiyya yakiendelea

Cha Kujifundisha katika Imani ili Tudumu katika Kufanya Vitendo Vizuri

Na **Abdulaziz Salum Disowile**

"*Inna lladhina aamanu waamilu swaalihati yahdiihim rabbuhum bi imaanihi tajrii min tahtihimu lánharu fii jannati nnaíim*"

Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, Mola wao Atawaongoza kwa sababu ya Imani yao. Itapita mito chini yao katika mabustani yenye neema (10:10)

Mwongozo wanapata wale wenye kuwa na Imani ya kweli na kufanya vitendo vizuri tu. Kwa hiyo hii ni habari njema kwa waaminio ambao Imani yao ni ya kweli na ni safi na wanafanya vitendo vizuri, hakuna shaka juu yao katika kupata muongozo. Imani na vitendo ni vitu ambavyo vinategemeana na kutegemeana kwake ndiko kunakomuwezesha mwaminio aweze kudumu katika kufanya vitendo vizuri mfululizo na katika hali ya kudumu kwa uimara. Kwa hiyo mtu mwenye Imani ya kweli na anadumu katika kufanya vitndo vizuri haiwezekani Allah Amuache bila Kumpa mwongozo au Amuache bila Kumuongoza ilia pate kudumu kwa uimara katika hali ya kufanya vitendo vizuri siku zote. Ndio kusema kwamba hata kama kuna udhia unapatikana katika njia ya Allah, udhia ule usiwaachisheni kufanya vitendo vizuri nyinyi wenye Imani safi, bali ombeni mwongozo kutokana na udhia ule kutoka kwa Allah ili Awaongozeni na ili mjue cha kukifanya katika hali hiyo ya udhia na Allah Atawaongozeni.

Na kutokana na mwongozo mtakaoupata ndio utakaowapa nguvu kwa kuondolewa wasiwasi na utawafanya muendelee kufanya vitendo vizuri mkiwa wenye utulivu na furaha bila kugawanyika kwenye makundi. Na hakuna yeyote ambaye ataomba mwongozo akakosa nguvu ya kuendelea kufanya vitendo vizuri eti kwa sababu ya udhia fulani uliojitokeza. Fahamuni ya kwamba Allah Anajua udhia huo kama Yeye Mwenyewe Alivyosema kuwa "ni Allah Ajuaye sana". Naye Akaleta kitabu ambacho ni mwongozo ambapo katika kitabu hicho kuna makatazo, maagizo na maamrisho ambayo yawezekana mwenye kuweka udhia anayajuwa lakini hawezi kuyafuata. Sote tunafahamu ya kuwa Allah Ameleya Quran kuwa mwongozo kama Anavyosema kwamba "*Hicho ndicho kitabu kisicho shaka ndani yake. Ni mwongozo kwa wamchao Allah*". Lakini pia Amesema kuwa "kama mkihitilafiana jambo Fulani basi lirudisheni kwa Allah" na ndio kusema kwamba katika maneno haya ndiyo yanatupa nguvu ya kuendelea kuomba mwongozo katika mambo mbalimbali ambayo aidha yawe ya kibinafsi ambayo hayahitaji mushawara au yale mliyoshindwa kuyapatia ufumbuzi au yale yanayoleta udhia katika njia yake au yale mliohitilafiana. Mambo ambayo yanaweza kutokea wakati wowote katika maisha yetu ya kila siku. Kwa mfano; mtu linaweza likamkuta jambo ambalo linampasa mshangao naye akabaki ameduwaa asiende mbele wala kurudi nyuma maana anajua akirudi nyuma atakuwa anakosea na shabaha yake ni kusonga mbele lakini akitaka kwenda mbele hajui njia gani apite ambayo itakuwa sahihi. Na mwingine anajitahidi kulazimisha kwenda mbele bila kujua kama anakosea au anapatia nap engine anakuwa na wasiwasi. Lakini kama mtaomba mwongozo basi mtaondolewa wasiwasi na mtapata nguvu na uimara wa kuendelea kufanya vitendo vizuri bila kuharibu Imani ya mtu. Ndio kusema kwamba ni kupitia muongozo ndio mtu anaweza kujua zuri na baya, katazo na agizo na kutokana na ufahamu huo wanaoupata kwenye muongozo ndio unaowafanya waaminio wanakuwa watiifu wenye kuacha kila aina ya ubaya na uovu na uasi na kuwafanya wadumu katika kufanya vitendo vizuri ambavyo ni matokeo ya kuwa na Imani nzuri, safi nay a kweli huku wakiwa makini kwamba wanafanya kila kilichoainishwa kwenye muongozo waliopewa.

Ifahamike ya kwamba Imani ndio ambayo inamtakasa mtu na utakaso ndio unaomwezesha mtu kufanya vitendo vizuri kwa Imani safi chini ya muongozo na ndio maana kabla ya kuanza kuswali, kutoa zaka, kufunga saumu na kuhiji ambavyo kimsingi ndio miongoni mwa vitendo vizuri, yampasa mtu aamini kwanza juu ya umoja wa Allah halafu akishakuwa na Imani ya kwamba hakuna Apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah tena aamini pasipo kumshirikisha na chochote, hapo sasa mwenye kuamini anaweza kuanza kufanya vitendo vizuri na vitendo hivyo vizuri ambavyo anavifanya chini ya imanisafi na ya kweli na kwa kufuata muongozo aliopewa hapo sasa vitendo vya mwenye kuamini ambaye sasa anaitwa mwaminio ndio vinapata kuwa na thamani mbele ya Allah kwani matendo matupu hayana thamani mpaka yamefuatana na utakaso wa moyo utakaso ambao kimsingi ndio Imani. Ndio kusema kwamba mtu ambaye anafanya vitendo tu bila Imani ni kama msafiri ambaye anasafiri bila lengo na wala anakokwenda hakujui na wala hana dira kwenye safari yake hapa sasa safari ya mtu huyo inakuwa sio safari bali ni kutangatanga.

Hebu tutizame mfano huu kwamba mtu anayetaka kuiba lakini anashindwa kutekeleza nia yake hiyo kwa sababu ya kukosa nafasi ya kufanya hivyo, mtu huyu huwezi kumuita mwaminifu. Hali kadhalika kama moyo wa mtu unaogopa vitu vingine minghairi ya Allah, ingawa haviabudu waziwazi mtu huyu hawezi kuitwa mchamungu kwelikweli. Kwa hiyo Islam inatilia mkazo kwenye vitu vyote viwili yaani Imani na vitendo vizuri. Wala haisemi kwamba kufanya vitendo vizuri tu bila ya Imani kuwa kunatosha, hapana. Na wala haisemi kuwa Imani tu peke yake bila vitendo vizuri kuwa inatosha, hapana. Bali mkazo unaotiliwa na Islam ni kwamba vitendo vyema lazima vifuatanae na Imani yaani kutakasika moyo. Maana inamkinika ya kwamba haiwezekani mtu mwenye moyo safi akakosa kufanya vitendo vizuri kwani moyo wa mtu hautawaliwi na jambo lolote la nje bali moyo wa mtu unatawaliwa na jambo la ndani ambayo ni Imani. Imani ndiyo inaratibu matendo yake kwa maana ya kwamba ukiona mtu anafanya vitendo vibaya basi ujue kabisa ya kwamba mtu huyo Imani yake ni mbaya na hawezi na hauwezi kumfanya afanye vitendo vizuri hata kama umpatie Quran Tukufu aisome yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho itaishia tu kujua makatazo, maagizo na maamrisho lakini hawezi kuifuata wala haiwezi kumpa athari yeyote ambayo itaweza kumshawishi kufanya vitendo vizuri Abadan. Hata kama mtu huyo aongee kwa busara na kwa uso wa tabasamu hali hii ya kuonyesha busara na tabasamu anaitumia tu kuficha makucha yake. Hali ambayo katika usemi wa kawaida tunaweza kusema kuwa, hii ni danganya toto ambayo inaweza kumuonyesha mtu kuwa kama vile mtu mzuri kwa mwonekano wan je kumbe huyo ndiye jambazi, haini, wizi, fasiki, mshenzi, mlafi, mroho, mzinifu, mzushi, muongo, mshirikina, tapeli, mfitini, na ni mwenye kilia aina ya uchafu na uasi, Imani yake mbaya na matendo yake mabaya ndipo waliposema Waswahili "*Busara zako za nini, kama hauna hata chembe ya wema!!?*"

Kwa hiyo fahamuni ya kwamba mtu hawezi kuficha Imani yake ikiwa vitendo vyake vinadhihirika na hata kama akifanya vitendo kwa kuigiza mbele ya watu na kuonyesha kuwa ni mwema, hataweza kudumu sababu Imani yake ni mbaya. Hivyo hawezi kuwa na vitendo vizuri na kuigiza kwake ni kuficha Imani yake mbele ya watu lakini je ataweza kuficha Imani yake mbele ya Allah? Na kufanya hivyo ni uwongo ambao machoni mwake mtu huyo anajiona kama amefanikiwa kumbe amejichimbia kaburi maana hana imani safi na hafanyi vitendo vizuri na hawezi kufuata mwongozo kwa sababu mwongozo unawafaidisha tu wenye imani safi na ya kweli na ndio ambao wanaweza kufanya vitendo vizuri. Kwa hiyo mtu aina hiyo adhabu ya Allah ni juu yake maana hawezi kubadilika hata umuonye vipi. "*Ni sawa kwake umuonye au usimuonye hataamini*" kwa maana hawezi kupata imani kwa kumuonya maana Allah Anasema ukumbusho unawafaa wenye imani safi yaani waaminio. Kwa hiyo adhabu ni sehemu yao ya msingi na ya lazima maana kila mmoja anastahili sawasawa, na adhabu ndio malipo ya mkosaji.

Allah Ameufanya mwongozo utegemee juu ya kitu ambacho kipo kabisa katika uwezo wa mtu mwenyewe yaani imani iwepo kabisa ndani ya moyo ndio mwongozo ukunufaishe. Ambapo, imani haiwezi kutawaliwa kamwe na watu wengine. Hivyo basi kwa kuongezea kwa sababu ya imani, vitendo vya mtu vinalipwa sawa na kiasi cha imani ya mtu. Kwa mfano; vitendo vya watu wawili vinaweza kuwa sawa na vyenye kupatana kwa mtazamo wa nje, lakini malipo yao yanaweza kuwa mbalimbali kabisa sawa na 1. Hitilafu ya vipimo vya imani yao, 2. Uaminifu wao na 3. Pendo lililochochea kufanya vitendo hivyo kwa maana hii kwamba, mwingine anasali, anatoa zaka, na anafunga saumu ili tu ajivike joho la wema kwa maana kwamba vitendo hivi anavifanya kichaka tu cha kufichia uovu wake na anafanya hivyo kwa kuigiza tu na sio kwa imani safi na anafanya hivyo ili aendelee kupata nafasi ya kuiba, kudanganya, kufitini na maovu mengine ikiwa ni pamoja na kuzuiliwa watu katika njia ya Allah. Allah Anasema "*wale wanaopenda maisha ya dunia kuliko akhera, na kuzuwilia watu njia ya Allah, na wanataka kuipotosha, hao wamo katika upotevu wa mbali*" (14:4). Lakini fahamuni ya kwamba onyo hili la Quran Tukufu, bali onyo hili la Allah haliwezi kumsaidia mtu huyo kwa sababu maneno haya matukufu ya Allah yapo kwenye muongozo ambao hauwezi kumsaidia mtu ambaye hana imani, kwa hiyo mtu kama huyo hawezi kuacha kufanya uovu bali ataendelea tu kufanya uovu basi tu ili muradi ametia udhia katika njia ya Allah. Tena vile vitendo anavyovifanya kwa kuigiza hafanyi kwa kumuogopa Allah, hapana! Maana imani yake ni mbaya na vitendo vyake pia ni vibaya. Na vitendo hivyo anavyovifanya kwa kuigiza anafanya hivyo lwa kuwaogopa viongozi wake ili wasije wakamharibia dhamira yake kwa hiyo mtu kama huyu hawezi kulipwa sala zake, zaka yake na saumu yake sawa na mwenye yule mwenye imani safi ambaye anafanya vitendo vyake kwa hofu ya Allah na kudumu kwake na bidi na juhudi na uimara wake ni kwa kutafuta radhi ya Allah. Kwa hakika jambo hili linafaa sana kukumbukwa kwa hiyo niwaombe na kuwanasihi wale wenye imani safi kutunza na kulinda vitendo vyenu na muipe nafasi imani yenu safi iendelee kutawala vitendo vyenu kwani hiyo ndio sifa ya waaminio ambao wanafanya vitendo vizuri ili wanapoelekea kwenye muongozo wanaopatiwa na Allah, uweze kuwafaidisha na kuwanufaisha maana yule mwenye imani mbaya au asiye na imani kabisa hawezi kufaidika na mwongozo kama Allah Anavyosema: "Hicho ndicho kitabu kisicho shaka ndani yake, ni muongozo kwa wamchao Allah". Kwa hiyo kitabu hiki cha mwongozo yaani Quran Tukufu kinawaongoza wale wenye imani safi yaani waaminio. Waaminio ambao wanamwamini Mungu mmoja na hawamshirikishi na chochote. Tujitahidi kuwa imara na kumtegemea Allah katika kilia jambo na tuendelee kudumu kwa uimara katika hali ya daraja la juu la uchamungu mpaka kufa kwetu. Insha Allah zile bustani zipitazo mito chini yake tuweze kuzirithi ambazo zitakuwa ni za kwetu moja kwa moja yaani itakuwa ni raha mustarehe. Huko hakutakuwa na udhia tena kwa maana ya kwamba hata kama heshima yenu ikadhulumiwa yote hapa duniani, Allah Atawapa heshima yenu huko peponi. Allah Atusaidie

Mapenzi Baina ya Waahmadiyya na Khalifa

Kutoka uk.12

Khalifa mtukufu anasema tena; wakati wa Ukhalifa wa pili pindi mwamko wa Shudhi ulipoibuka. (mwamko wa dini ya kibaniani uliowashawishi waislamu kuacha dini yao na kuingia katika Uhindu). Khalifa Mtukfu wa Pili r.a. katika mwaka wa 1923 alitengeneza mpango akiwahimiza waahmadiyya kwenda sehemu zile mbali mbali zilizokuwa na athari hiyo kwa kujitegemea ili waweze kuwahubiri na kuwarejesha katika Islam. Watu kutoka nyanja mbalimbali walijitolea na kwenda kufanya mahubiri huko, na watu wengi walisilimu na kurejea katika dini ya Kiislam.

Khalifa mtukufu wa Pili r.a. mwaka 1924 alikuwa safarini katika nchi za Ulaya. Upweke huu wa muda uliwafanya wanajumuiya wahisi huzuni kubwa. Mtu mmoja anaandika "Ee mpendwa wetu, sisi tuko mbali na wewe, nasi tumelazimika kuwa hivyo, kama ingewezekana basi sisi tungekuwa mavumbi chini ya miguu yako. Mimi sijawahi kwenda Qadian kwa miaka minne, lakini nilikuwa na imani na tumaini nitakapokwenda Qadian nitakwenda kubusu miguu yako. Lakini sasa hata siku moja kwangu ni ngumu. Allah Ajaalie Khalifa mtukufu arudi Qadian haraka kwa amani.

Khalifa mtukufu wa Pili r.a. anasema; kijana moja bila ya hati ya kusafiria alifika Afghanistan, naye akaanza kuhubiri. Serikali ikamtia ndani. Ndani ya jela akaendelelea kufanya mahubiri na baadhi ya watu wakaanza kuathirika. Maafisa wakatoa taarifa, masheikh wa kisunni wakatoa fatwa ya kuuawa kwake. Lakini waziri akasema huyu ni raia wa Kiingereza kwa hiyo wakamrudisha India. Akarudi baada miezi mingi. Angalieni jazba na ujasiri wake, nilipomuambia kuwa ulikosea, ungeweza kuhubiri bila ya kukamatwa pia. Akajibu niambie nchi yeyote niende nikahubiri. Kama vijana wengine waoneshe jazba kama hii wanaweza wakaibadilisha dunia mara moja.

Bwana mmoja kutoka katika nchi ya Syria anayeitwa Muhammad As-Shifa, ambaye ni wakili alikuwa na uhusiano madhubuti na Ukhalifa. Kwa kuwa alikuwa ni wakili alipenda kila jambo lithibitishwe kwa dalili, lakini jambo lolote linaposemwa kuwa limetoka kwa Khalifa wa zama basi jambo lile lilikuwa kama amri isiyo na mjadala.

Kulikuwa na mwanamke mmoja zama za Khalifa wa Tatu, yeye alikuwa anapenda Ukhalifa na Khalifa kiasi kikubwa sana. Alikuwa anachukulia utii kwa Khalifa kuwa jambo la kwanza. Wakati Khalifa alipokuwa katika ziara nchini Marekani alisikia hotuba yake iliyohimiza uvaaji wa hijab, mara moja alianza kuvaa hijabu. Katika zama zile yeye alikuwa ni mwanamke pekee katika eneo lake aliyekuwa anavaa hijab.

Kuna tukio moja linalomhusu Ahmadiyya mmoja Bw Mukhtar Ahmad. Mwaka 1974 nchini Pakistan hali ya upinzani ilimuondolea raha na utulivu. Yeye aliuza ardhi yake na kuhamia Rabwah kwa ajili ya elimu bora ya watoto wake. Alipoonana na Hadhrat Khalifa tul Masih wa Tatu rh. akamueleza kuwa aliuza ardhi yake kule nyumbani kwao na akakodi ardhi pale Rabwah. Khalifa Mtukufu r.a. hakupendelea jambo hili la kuuza ardhi yake nyumbani. Ikabidi arudi tena nyumbani kwao na kumpa taarifa Khalifa mtukufu kuwa ametekeleza amri yake. Khalifa mtukufu alionesha furaha yake.

Khalifa mtukufu wa Tatu r.a. anasema; kulikuwa na mpango mmoja ambapo mimi ilibidi nisafiri maili mia moja kwenda kutoa hotuba. Kule walikuwapo Wakristo wageni. Kwa hiyo muda mrefu ulitumika kwa ajili ya hotuba na maswali na majibu kiasi kwamba kwa sababu ya kuchelewa niliwaambia hatutapeana mikono. Watu wale ambao miaka mingi walikuwa hawajamuona Khalifa, wakasimama na kumkimbilia kwa ajili ya kupeana mikono. Kwa hiyo kwa taabu kubwa sisi tuliondoka pale. Alisema jambo hili nasema kuwaambia watu wengine wasiokuwa Waahmadiyya lakini sisemi kwa Waahmadiyya, kwani mimi sio mjinga kuwa nianze kufikiria kwamba mapenzi haya ni kwa sababu ya ubora na sifa yangu; bali mapenzi haya yametiwa mioyoni na Allah pekee. Katika zama za Khalifa wa Nne mabadiliko makubwa yaliyotokea, ni kwa sababu ya kujitolea kwa wabashiri wa zamani. Inasemekana baadhi ya Waahmadiyya wenye uzoefu wa muda mrefu wamesema kuwa katika jamaat mapenzi yamezidi kiasi kwamba yamevuka mpaka wala sisi hatuwezi kuwa na makadirio yake. Sisi hatukuwa na dhana yoyote kuwa watu wetu sisi wangepata nafasi ya kutoa huduma kwa Khalifa mtukufu. Mambo haya yote yameletwa na Allah pekee.

Khalifa mtukufu anasema; sasa nitazungumzia juu ya matukio ya zama zangu. Katika mwaka 2004 nilifanya ziara nchini Nigeria. Hakukuwa na mpango wa kwenda kule lakini tulipofika tukagundua kuwa kulikuwa na umuhimu haswa wa kwenda. Kabla ya kwenda kwetu tayari mkutano wa mwaka (Jalsa salana) ulikwishafanyika. Wala hatukufikiria kwamba watu wengi wangekuja kuonana nami, lakini watu waliokuja walifikia 30,000. Mapenzi na uhusiano wa kweli tuliouona hausemeki. Wakati wa dua watu walilia kwa unyenyekevu na uchungu mkubwa kiasi cha kushangaza. Mapenzi kama haya huwa yanaletwa na Allah tu. Masheikh wa kisunni wanasema sisi tumefunga harakati za kimahubiri za maqadiani Afrika. Mtu yeyote awaulize kuwa yale mapenzi na ikhlas wanayoionesha watu, yale yanayooneshwa na MTA, na yale tunayoyaona kule baada ya kwenda; mambo haya yote ni nini? Je, haya ni matokeo ya kufunga harakati za kimahubiri?

Mwaka 2008 nilizuru Ghana. Jumuiya ilikuwa imenunua eka 500 za ardhi; kule ndiko ulikofanyika mkutano. Kulikuwa na mabanda ya kuku. Ambayo yalibadilishwa na kuwa sehemu ya kuishi wageni wakati wa Jalsa. Lakini hata hivyo kulikuwa na uchache wa sehemu ya makazi, lakini hakuna hata mmoja aliyelalamika. Ingawa miongoni mwa watu waliokuja walikuwemo matajiri na wenye kipato kikubwa, kama walikosa sehemu ya kuishi walitandika miswala nje na kulala kule. Watu hawa walionesha subira kubwa. Mtu mmoja akawauliza baadhi yao je, ninyi mlipata taabu sana kule? Wakajibu sisi tulikuja kushiriki katika Jalsa, na Jalsa hii inafanyika huku Khalifa mtukufu^{atba} akiwa amehudhuria. Taabu hii ya siku mbili tatu inadhuru nini. Sisi tunafuraha ya kwamba tumeweza kushiriki katika Jalsa.

Watu kutoka nchi ya Burkinafaso pia walifika. Nikapata taarifa kuwa baadhi yao hawakupata chakula. Khudaam 300 walifika baada ya kusafiri kilomita 1600. Walipofikishiwa ujumbe wa kuwaomba radhi kwa kukosa kwao chakula, walijibu, lile lengo lililotuleta tumelipata. Chakula cha kiroho kama hiki tutapata wapi kila siku. Jumuiya ya Burkinafaso si ya siku nyingi lakini wao wanasonga mbele katika kuonesha mapenzi makubwa. Baadhi ya watu ni maskini kiasi kwamba walikuja wakivaa jozi moja tu ya nguo na wakashinda nayo siku tatu au wiki bila ya kubadilisha. Walifika mkutanoni kwa kuunga-unga nauli. Khuddam ul Ahmadiyya waliokuja kwa baiskeli, walifika kusimama na kupumzika sehemu mbali mbali njiani wakisafiri kwa siku saba. Baadhi ya watu miongoni mwao walikuwa wazee wa miaka 50 au 60 na wawili walikuwa ni watoto wenye umri wa miaka 13. Mtu fulani akawaambia bila shaka mlipata taabu kubwa. Wakajibu waislamu wa kwanza walijitolea kiasi kikubwa sana, tulikuwa tunapenda vijana wetu wawe tayari kujitolea katika kila hali. Sisi tumefanya safari hii kwa ajili ya kutoa shukurani kwa sababu ya kupata Ukhalifa.

Baadhi ya sehemu ufakiri na umaskini umewafanya wawe na maisha mabaya. Lakini baada ya kuingia katika jumuiya ya Mtume^{saw} wamepata ikhlas na mapenzi ya kweli.

Basi tunatakiwa kuendelea kuomba ili Allah Ayafanye mapenzi haya yawe ya milele na milele.

Khalifa mtukufu anasema; ndugu mmoja kutoka Burkinafaso anasema, mimi nimefanya baiat miaka mitatu iliyopita. Ni leo nimekuja kufahamu kuwa mimi nimefanikisha kitu gani. Kwa sababu leo nimemuona Khalifa furaha yangu haiwezi kuelezeka.

Mwaka jana fasidi mmoja alijitahidi kueneza fitna. Baadhi ya vijana waliathirika naye. Wao katika kujieleza walikuwa wanasema wao ni waahmadiyya lakini ukweli ni kuwa wao walikwishaanza kuwa mbali na nidhamu ya Jamaat. Mbashiri mmoja kutoka nchi ya Mali akapelekwa. Yeye akawaeleza kuwa ninyi mmefungamana na Ukhalifa nanyi mnajitenga mbali na nidhamu ya Jamaat. Karibu wote wakaandika barua ya kuomba radhi. Wakasema sisi tuliathirika na mambo haya kutokana na uchache wa malezi na kwa sababu ya kuelewa vibaya. Sisi tunao uhusiano wa kweli na Ukhalifa.

Ndivyo ilivyo hata kule Gambia na Ivory-Coast kila mmoja sawa na uwezo wake amesonga mbele katika uhusiano na Ukhalifa.

Katika nchi ya Ghana wakati wa Jalsa sehemu ya kuishi ilikuwa mbali na uwanja wa mkutano, karibu kilomita moja. Njiani watu, wakina mama na watoto walikuwa wanasimama kusalimia. Walikuwa wanaonesha mapenzi yao kwa Khalifa. Idadi ya wakina mama ilikaribia 50,000. Mapenzi yao yalikuwa yanatiririka kutoka katika kila sehemu, usoni na machoni. Nao walikuwa wanahudhuria bila kukosa katika sala za Tahajjud na zile za kawaida.

Nilipokwenda Nigeria kwa mara ya pili, ilibidi kusimama sehemu moja ambapo msikiti mpya ulikuwa umekwishajengwa ili kwenda kuutazama. Kule watu walikusanyika nao walitaka kusalimiana kwa kupeana mikono na wanawake walitaka wamuone Khalifa kwa karibu. Kwa sababu ya uchache wa muda jambo hilo halikuwezekana. Wale waliojitahidi kusonga mbele waliweza kusalimiana nami. Katika foleni mtu mmoja akamwambia mwingine rudi nyuma kidogo. Mwanamke mmoja akajitokeza na kumwambia; wewe ni nani uwe kikwazo kati yangu mimi na Khalifa.

Khalifa mtukufu anasema watu wanaichukulia Amerika kuwa watu wake ni wapenda dunia, wana uhusiano mchache na dini. Kila mara nilipokwenda kule nilishuhudia watu wakidhihirisha mapenzi ya kweli. Jambo hili linapinga ile fikra kuwa wao ni wapenda dunia tu. Vijana waliokuwa wanahudumu katika kitengo cha ulinzi walibaki nami muda wote. Wao walikuwa nami safarini bila kujali kupoteza kazi yao na biashara zao. Baadhi yao waliacha kabisa kazi yao na kuja kuwa nami safarini. Mapenzi na ikhlas hii ya kweli haiwezi kuletwa na mtu bali ni kazi ya Allah.

Mimi nilitoa hotuba kuhusu utii na ikhlas kwa Ukhalifa katika nchi ya Ujerumani. Hotuba ile ilikuwa ni kwa ajili ya kila mmoja. Kwa neno zima watu wote wa dunia nzima walionesha kuitekeleza, na wakaonesha utii na mapenzi makubwa ya kweli kwa Ukhalifa. Hususan baadhi ya watu wenye majukumu ya uongozi wakasema baadhi yetu tulikuwa tunatoa tafsiri zetu za amri tulizokuwa tunapewa, kutoka sasa haitakuwa hivyo.

Kutoka Jordan bwana mmoja anaandika kuwa hii ni dalili kubwa ya ukweli wa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} kwamba mapenzi ya UKhalifa yamekuja yenyewe moyoni. Katika ndoto Allah Amenionesha kuwa Khalifa mtukufu anafanya kazi ya kusuluhisha magomvi na kueneza amani, mimi niliweka mkono wangu juu ya mkono wake na kubusu pete yake, ndipo nilipohisi na kusikia mapenzi ya kweli. Mimi ninataka kufanya baiat upya kwako, na kuahidi kuwa mbali na kila yule asiyekutii.

Katika nchi ya Bulgaria tayari jumuiya imeanzishwa. Kila mmoja ana mapenzi ya kweli na Ukhalifa.

Khalifa mtukufu anasema mimi nimekwishatoa mifano michache inayothibitisha kuwa mapenzi ya kweli kwa Ukhalifa anayaleta Allah peke yake, na hakuna nguvu yeyote inayoweza kuyaondoa. Ninyi mtaendelea kushuhudia ahadi ya Allah ikitimia. Allah Ajaalie wengi wetu kupata mapenzi haya.

Kuhusu MTA pia naomba nitoe matangazo. Toka tarehe 27 Mei, siku ya Ukhalifa kuna utaratibu mpya ulioanzishwa. Sawa na maeneo channel za MTA zimebadilishwa katika sehemu nane. MTA1 itatangazwa katika Kiingereza na Kiurdu. MTA2 ni kwa ajili ya Ulaya na Mashariki ya Kati, kutakuwa na channel kwa ajili ya Kiurdu, Kijerumani, Kituruki na Kiajemi. MTA3 AL-ARABIA itakuwa katika lugha ya Kiarabu. "MTA4 Afrika" itakuwa kwa ajili ya Afrika katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. "MTA 5 Africa" hii ni kwa ajili ya nchi za Afrika Magharibi. "MTA 6 Asia" ni kwa ajili ya bara la Asia, Japani na Urusi. Itatumia lugha ya Kiurdu, Kiingereza na Kiindonesia. "MTA 7 Asia" itakuwa Channel ya HD, hii ni kwa ajili ya India, Pakistan na Bangladesh. Lugha itakayotumika ni Kiurdu, Kibengali na Kihindi, pia Kitamili na Kimalialam. Na Channel nyingine itakua "MTA 8 America".

Allah Atie Baraka katika utaratibu huu.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jum. II - Raj. 1440 AH | MACHI 2020 | AMMAN 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

"Mtume[saw] alikuwa anasema, "Pengine unalazimika kutoa sadaka, lakini hutoi, basi haramu inaangamiza mali yako ya halali. Bila shaka haramu haichanganyiki na halali ila inaihilikisha." (**Kashf-ul-Gumah**)

Mapenzi Baina ya Waahmadiyya na Khalifa

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 29/05/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad[atba] ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema;

Masihi Aliyeahidiwa[as] katika sehemu moja anasema; mimi namshukuru Allah kwa kuwa amenipa Jumuiya yenye ikhlas na mapenzi ya kweli. Mimi ninaona kazi ninayowaitia wanakuja kuifanya haraka na kwa jazba kubwa kila moja akishindana na mwingine kuwahi sawa na uwezo wake. Mimi ninaona ndani yao ikhlas na upendo wa kweli.

Sisi pia tumeshuhudia ikhlas na mapenzi hayo kwa Masihi Aliyeahidiwa[as] Kuna matukio mengi ya maswahaba wake. Kuna simulizi nyingi katika familia za Waahmadiyya wa zamani, na mambo haya pia yamo katika vitabu vyetu. Lakini uhusiano huu uliokuwepo kwake unaendelea kupatikana katika familia za jamaat na katika wale wanaojiunga na jamaat sasa. Na ndivyo inavyotakiwa. Uhusiano huu mwema na wa kweli haukubaki kwao tu, bali mnyororo huu sawa na ahadi ya Allah unaendelea kuwa madhubuti katika watu wa zama za leo. Ni uhusiano huu ambao ni alama ya umoja wa jumuiya. Masihi Aliyeahidiwa[as] alitoa habari ya kifo chake kwa jumuiya, pamoja na hayo akatoa habari njema baada ya kupata ufunuo kutoka Allah ya kuja kwa Ukhalifa.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema; msihuzunike wala nyoyo zenu zisifadhahike kwa sababu ya jambo langu hili, kwa sababu ni juu yenu kuiona kudra ya pili, kwani itabaki kuwa ya milele. Hiyo haitakuja mpaka mimi nitakapoondoka. Lakini mimi nitakapokuwa nimeondoka Allah ndipo atakapoileta, nayo itabaki nanyi milele kama ilivyoahidiwa. Kama Allah anavyosema; Mimi nitawafanya wafuasi wako kuwa juu ya wengine mpaka siku ya Kiyama. Basi kwa fadhili ya Allah sawa na ahadi yake Ukhalifa ukaanzishwa. Kuendelea kwa nidhamu hakuna maana yeyote mpaka kuwepo uhusiano wa kweli, ikhlas na upendo baina ya wanajumuiya na Khalifa. Nao unaletwa na Allah pekee. Hakuna mtu wala juhudi yake inayoweza kuleta uhusiano huu.

Khalifa Mtukufu anasema; uhusiano uliopo baina ya Khalifa na wanajumuiya, ndio ushahidi wa kutimia kwa ahadi ya Allah, nayo ni dalili ya nusra na msaada wake kwa Masihi Aliyeahidiwa[as] nayo ni dalili ya ukweli wa jumuiya. Na katika uhusiano huu watu wote wanashiriki, wale wa zamani, wapya, vijana, watoto, wazee, na akina mama. Pamoja na wale watu wanaoishi mbali ambao hawajawahi kumuona Khalifa, hawa wote wanashiriki. Nao wako tayari kutekeleza amri na maagizo yake yote. Haya si maneno matupu bali kuna matukio kadhaa wanajumuiya wanayaonesha. Kama matukio haya yaandikwe katika vitabu basi ni majalada chungu nzima yatapatikana.

Khalifa mtukufu[atba] anasema sasa nitazungumzia baadhi ya hisia na matukio hayo.

"Mhariri wa gazeti la Al-Badr kuhusu kuumwa kwa khalifa wa kwanza r.a. anaandika kuwa barua za makhuddam zinakuja. Khalifa mtukufu wa kwanza akajibu mimi ninawaombea dua wale wote wanaoandika barua. Mhariri anasema mtu mmoja anaandika kuwa; mimi nimeomba dua kwa Allah, Ee Mola wangu kwa ajili ya mahitajio mbali mbali ya Jamaat Umjaalie Khalifa wetu maisha marefu kama yale ya Nuhu[as] Mtu Mwingine anaandika, baada ya kusikia hali njema ya afya ya Khalifa mtukufu moyo wangu ulipata furaha ya ajabu.

Endelea uk 11

KITABU

SIRI YA UHAKIKA

Na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

Siri ya Uhakika

This book was published in 1898. In this book, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad of Qadian, the
Promised Messiah and Mahdias, has shed light on the true life history of Jesus Christ and explained, with historical evidence, that Jesus, son of Mary, had survived crucifixion and migrated to India where he died at the age of 120 and was buried in the Khanyar quarters of Srinagar, Kashmir. A sketch of his shrine in Srinagar has also been given in the book.
The later half of the book is largely devoted to the refutation of criticism made by Maulawi
Muhammad Husain regarding the language of an Arabic revelation of the Promised Messiahas. The Promised Messiahas has answered the objection with logical and rational arguments quoting examples from the traditions of the Holy Prophet, peace and blessings of Allah be upon him, and renowned poets of Arabia, and proved that divine revelation was beyond reproach and fulfilled all the requirements of Arabic grammar.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba Tsh 3,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com